



Kusema kwangu: Sub-haanallaah, na Alhamdulillah, na Laa ilaaha illa Ilaah, na Allaahu Akbaru, kunapendeka sana kwangu kuliko vitu vyote vilizochomozewa na jua

Imepokewa kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Allah ziwe juu yake- amesema:
Amesema Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake-: "Kusema kwangu: Sub-haanallaah,
na Alhamdulillah, na Laa ilaaha illa Ilaah, na Allaahu Akbaru, kunapendeka sana
kwangu kuliko vitu vyote vilizochomozewa na jua".

[Sahihi] [Imepokelewa na Imamu Muslim]

Anaeleza Mtume -Rehema na amani ziwe juu yake- kuwa kumtaja Allah Mtukufu kwa maneno haya matukufu ni bora kuliko dunia na vilivyomo, na utajo huo ni kusema: "Sub-haana Ilaah": Ni kumtakasa Mwenyezi Mungu kutokana na mapungufu. "Alhamdulillah": Ni kumsifia kwa sifa za ukamilifu pamoja na kumpenda na kumtukuza. "Laa ilaaha illa Ilaah": Hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu. "Allaahu Akbaru: Mkubwa na Mtukufu kuliko kila kitu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/6211>

